Karatasi ya maelekezo jinsi ya kuanzisha biashara yako

Starting Your Own Business - Swahili

Je, wazo la biashara ni zuri?

Kuanzisha biashara ni jukumu kubwa. Kitu cha kwanza cha kuhitaji wakati unapofikiria kuanzisha biashara ni kujiuliza kuwa wazo hili la biashara ni zuri au inafaa? Biashara hii italeta faida?
Kufanya utafiti wa sehemu utakayo kwenda kuanzisha biashara ni kitu cha mhimu. Chunguza mtakao kuwa mnashindana kibiashara. Je kutakua na soko katika biashara yako na soko hilo litakuwa na ukubwa gani? Bei gani utakayo tumia na njia zipi utakazo tumia kutangaza biashara yoko?

Pale utakapokua umeona kuwa wazo la biashara ni nzurisana,yakupasa ukumbuke kuwa katika biashara kunakupata hasara na unachotakiwa ni kutafuta mbinu za kuzikabiri hasara hizo.Hata kama umeajiri wafanyakazi,umepanga sehemu ya kufanyia biashara na hasara za utawala wa kibiashara.

Unatakiwa uwe na mipango ya biashara jinsi ya kuanzisha biashara na jinsi utakavyoiendesha. .Mipango ya biashara ni nyaraka ambazo huelezea biashara yenyewe, malengo yake, mipango, soko linalolengwa na matarajio ya kipesa.

Kuchagua muundo wa biashara

Utatakiwa kuchagua muundo wa biashara yko kabla hujaanzsha hiyo biashara.Na kuna sheria zinazo hitajika kwa kila muundo wa biashara ambazo unatakiwa uzitumie. Aina za miundo ya biashara ni kama ifuatayo;

- Muundo wa biashara ya pekee
- Muundo wa kuingia ubia na mwenzio
- Muundo wa kuwa mwaminifu
- Muundo wa ushirikiano
- Muundo wa kushirikiana

Utatakiwa uombe ushauri kwa mhasibu anayehusika na miundo ya biashara juu ya muundo unaokufaa wewe.

Kukubaliana na sheria za Kiaustralia

Utatakiwa biashara yako iendeshwe kutokana na sheria za Kiaustralia.

Kwanza, unatakiwa ufanye usajiri sehemu zote husika. Unatakiwa ufanye usajiri wa jina la biashara yako katika sehemu ya usajiriwa majina Australia magharibi katika kitengo cha biashara. Kama muundo wa biashara yako ni Kampuni, hapo utatakiwa usajiri pamoja na wenzako chini ya hisa za kiaustralia na tume ya uwekezaji. Pia utatakiwa kuzingatia njia za kujisajiri jina katika mtandao wa miliki za majina au alama za biashara, kwa mfano alama utakayo tumia kutofautisha biashara yako na wengine.

Pia biashara yako itatakiwa isajiriwe kiserikali kwa kuwa na leseni na ruhusa ya biashara. Serikari ya mtaa,serikari kuu na shirikisho la kiserikari kila moja ina leseni husika na ruhusa zinazotakiwa kutokana na aina ya biashara. Leseni za biashara ya pamoja na ruhusa ni kama vile leseni ya shughuli za kazi za nyumbani kama vile biashara yako utaifanya katika eneo lako unaloishi, kufanya kazi na watoto angalia kama unaweza kufanya kazi na watoto, na kuwa vyeti vya polisi vya kitaifa vya kutokuwa na makosa

Australia ina utata katika utozaji wa kodi na ndipo utatakiwa uombe msaada kwa mwanamahesabu kuhusu shida ya biashara unayoweza kuwa nayo. Pia mwanamahesabu anaweza kukusaidia muundo wa kupunguza kodi na kuepukana na faini mbalimbali za

KANUSHO: Maelezo ya karatasi hii yanatoa mwongozo wa jumla tu na yasitumiwe badala ya ushauri wa kisheria. Kwa kiwango cha juu kinachoruhusiwa na sheria, CASE kwa wakimbizi Inc. inakanusha hasara yoyote ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja itakayompata msomaji ikihusiana na kutegemea au kuhusiana na maelekezo katika karatasi hii. Msomajai lazima apate ushauri wa kisherai kutokana na mazingira yake binafsi.

kodi,kwa mfano aina za kodi ambazo utatakiwa ulipe ikiwemo kodi ya kipato na kodi ya biashara

Kuna sheria ngumu eleweka za sehemu ya kufanyia kazi kuanzia mikoa na serikari kuu hapa Australia. Kama unadhamiria kuajiri wafanyakazi basi hauna budi kufuata sheria za Australia, kwa mfano kuna kiwango cha chini cha wafanyakazi na kiwango cha mshahara.

Hapo juu ni historia fupi ambayo inahusu mambo gani utatakiwa ufanye ili biashara yako ifanyike kwa kufuata kanuni na sheria za serikali.

Mikataba

Katika ufanyaji mzima wa biashara yako, unatakiwa kuingia kwanye mikataba. Mkataba ni makubaliano ya kisheria yanayofanywa na pande mbili au zaidi ambayo huleta busara au maamuzi ya kufanya kitu au kutokufanya kitu.

Sheria inayo husika na mikataba ni ngumu na mwanasheria anaweza kukusaidia kujua au kukuandalia mkataba badala yako. Miongoni mwa vitu vingine, unatakiwa uwe unaelewa mkataba mzima na ukubaliane na masharti yake kabla ya kusaini mkataba huo.

Bima

Hakikisha biashara yako inakuwa salama na inahifadhiwa mbali na matukio yasio makusudi kama vile, kupoteza au kuharibika kwa rasilimali za biashara nafaida, madai ya kisheria kutoka kwa wateja na ajira za waajiri wako. Mfano wa bima ni kama vile bima ya gari, bim ya hasara na bima za fidia za wafanyakazi

Unatakiwa kuomba msaada kwa wakala wa bima kulingana na aina ya bima inayotakiwa katika biashara yako

Kupata Ushauri kutoka kwa wahusika Mahiri

Kuna watu wengi ambao wanaweza kukusaidia kuimarisha biashara yako. Mshauri biashara anaweza kukusaidia biashara yako na kukuepusha njia za biashara yako ikuwe, Mwanasheria anakusaidia wewe hasa katika mambo yako ya kisheria na mikataba inayohitajika, mhasibu anakusaidia kwa mambo yote ya kifedha katika biashara yako, wakala wa bima awezakukusaidia katika kuchangua bima.

Ushirika wa kimaendeleo wa biashara ndogondogo sehemu ya serikali ya Australia Magharibi, unatoa msaada wa kijumla na kusaidia wamiliki wapya na wazamani juu ya biashara.

Wapi pa kupata msaada?

CASE kwa wakimbizi inc. ni taasisi isiyo ya kiserikali na sio ya kidini ambayo inasaidia wahamiaji na shughuli zote za kisheria katika mila na isimu ya Lugha(Cald)katika jamii ya Australia magharibi. CASE kwa wakimbizi inc. inaweza kukusaidia kwa ushauri na namna ya kuanzisha biashara yako.

Huduma zote sio za malipo, ingawa misaada ya watu binafsi na mashirika inapokelewa kwa ukarimu. Michango yote ya zaidi ya AUD $2.00 haina vati.

Mawasiliano ya CASE kwa wakimbizi inc. ni haya yafuatayo:

145 Stirling Street, Perth
Western Australia 6000

Simu:(08) 92277311

Kinukushi: (08) 92277188

Email:admin@caseforrefugees.org.au

Case for refugees

KANUSHO: Maelezo ya karatasi hii yanatoa mwongozo wa jumla tu na yasitumiwe badala ya ushauri wa kisheria. Kwa kiwango cha juu kinachoruhusiwa na sheria, CASE kwa wakimbizi Inc. inakanusha hasara yoyote ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja itakayompata msomaji ikihusiana na kutegemea au kuhusiana na maelekezo katika karatasi hii. Msomajai lazima apate ushauri wa kisherai kutokana na mazingira yake binafsi.